



Dira na mdogo wake walikuwa wakigombania mdoli mwenye umbo la Tembo mdogo wa plastiki. Tembo huyo alikuwa wa Dira.

Hivyo Dira alimsukuma Chaku.



Mama alimwambia Dira,
"Ujifunze kucheza na
mdogo wako vizuri."

Dira alikasirika alikimbilia
chumbani kwake. Alipanda
kitandani, akajifunika shuka
hadi kichwani akalala.




Dira aliamka asubuhi na mapema.
Alishangaa alipoona kuwa mama yake
hayupo. Alijaribu kuita lakini hakuweza
kumsikia akiitikia.





Dira alikwenda kwa mdogo wake. Chaku alikuwa na vitu vingi vya kuchezea. Chaku alikuwa na mipira na midoli mingi. Kaka yake hakuwa na kitu.

Chaku alikuwa na viatu vipya. Dira hakuwa na viatu.



Dira na mdogo wake walitoka nje. Walitembea barabarani. Barabara ilijaa Tembo!

Dira aliwakimbilia Tembo, alibembea kwenye mikonga yao, na aliwapanda migongoni.



Alicheza na kucheza, ila mdogo wake alikuwa amekaa peke yake.

Ghafla! Dira aliona Tembo mmoja anamfuata mdogo wake pale alipokaa.

Chaku alisimama na kuanza kukimbia.






“Chaku! Chaku!” Dira alipiga kelele.

Tembo walimfukuza. Alimuona mdogo wake akipanda mti. Alikaa kwenye tawi la mti huku akihema kwa nguvu.

“Dira!” mdogo wake alimwita kwa nguvu. “Tafadhali nisaidie!”

Dira alimpeleka kwa haraka Tembo
wake kuelekea mdogo wake aliko.
"Acha!" Alimpigia kelele yule Tembo.





“Usimumize!” Tembo walianza kula majani na wengine kuvunja matawi ya miti.



Dira aliruka kutoka kwa
Tembo hadi kwenye mti.

“Nishike mkono wangu!”
Alimwambia Chaku.

Wakati anataka kuushika mkono wa mdogo wake, Tembo mmoja alimnyanyua Dira na kumweka kwenye mkonga wake na kumtoa kwenye mti. Tembo yule akamrusha Dira juu.





Dira alianza kuanguka na kupiga kelele kwa sauti, "Mama tusaide!"

Ghafla Dira aliamka.

“Dira usiogope! Lazima ulikuwa unaota ndoto ya kutisha.”

Mama yake alimkumbatia. Chaku alikuja kuangalia nini kimempata kaka yake.





This book was made possible by Pratham Books' StoryWeaver platform. Content under Creative Commons licenses can be downloaded, translated and can even be used to create new stories - provided you give appropriate credit, and indicate if changes were made. To know more about this, and the full terms of use and attribution, please visit the following [link](#).

Images Attributions:

Page 12: [Two boys on tree branches](#), by [Godwin Chipenya, John William](#) © Room to Read, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license.

Page 13: [An elephant trunk grabs a boy](#), by [Godwin Chipenya, John William](#) © Room to Read, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license.

Page 14: [Boy falling down from a tree](#), by [Godwin Chipenya, John William](#) © Room to Read, 2014. Some rights reserved. Released under CC BY 4.0 license.

Page 15: [Boy wakes up from a nightmare, a woman and a child nearby](#) by [Godwin Chipenya, John William](#) © Room to Read, 2014. Some rights reserved.

Released under CC BY 4.0 license.

Disclaimer: https://www.storyweaver.org.in/terms_and_conditions




Some rights reserved. This book is CC-BY-4.0 licensed. You can copy, modify, distribute and perform the work, even for commercial purposes, all without asking permission. For full terms of use and attribution, <http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>



This book was made possible by Pratham Books' StoryWeaver platform. Content under Creative Commons licenses can be downloaded, translated and can even be used to create new stories - provided you give appropriate credit, and indicate if changes were made. To know more about this, and the full terms of use and attribution, please visit the following [link](#).

Images Attributions:

Disclaimer: [https://www.storyweaver.org.in/terms and conditions](https://www.storyweaver.org.in/terms_and_conditions)



Some rights reserved. This book is CC-BY-4.0 licensed. You can copy, modify, distribute and perform the work, even for commercial purposes, all without asking permission. For full terms of use and attribution, <http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>